

HATUA>> Februari 20, mwakani minada ya mifugo isiyosajiliwa kufun

*Waziri atoa angalizo kwa wafanyabiashara wa mifugo

Na JUMANNE GUDA

SERIKALI imesitiza kwamba minada yote ya mifugo inapaswa kusajiliwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvu, huku ikitahadharisha kuwa isiyosajiliwa itafutwa.

Waziri wa Mifugo na Uvuvu, Mashimba Ndaki, alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, alipozungumza na wafanyabiashara wa mifugo mkoani humo.

Kwa mujibu wa Waziri Ndaki, kumejitoza tabia ya kuanzishwa kwa minada mingi ya mifugo, bila ya kusajiliwa na wizara hiyo.

"Tiflako Februari 20, mwakani minada kama hajasajiliwa itafungiwa na kufutwa kwa mujibu wa sheria zilizoko za mifugo. Minada ya awali, ya upili na ya mipakani lazima isajiliwe na Wizara ya Mifugo na Uvuvu," alisema.

Kutokana na hilo, alizigiza mamlaka za senkali za mitaa kuhakikisha zinasajili minada yao huku akisitiza kama hajasajiliwa wapeleke maombi wizarani ili ikasajiliwe.

Katika hatua nyingine, Waziri Ndaki alipiga marufuku uanzishwaji wa machinjio, minada na mabucha bubu na kulagiza Bodii ya Nyama kuwachukulia hatua za kisheria wanajihushisha na mambo hayo.

Ndaki alisema kumekuwa na uanzishwaji wa machinjio na mabucha kiholela bila kusajiliwa na wizara na taasisi zake na kusababisha kero.

"Utakata machinjio yanakuwa bucha la nyama na hapo hapo unakuwa minada, ifahamike kuwa nyama ikitoka machinjioni ipelekwe katika mabucha ikauze. Machinjio yasigeuke kuwa bucha wala yasiwe minada," alisema.

Katika hatua nyingine, Ndaki alisema atawasiliana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuona namna ya kupunguza tozo za usafirishaji wa mifugo kutoka katika Halmashauri.

Alisema warnepokea malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara ya mifugo na bidhaa zake kuwanatozwa tozo nyingi, hivyo warneomba wapunguziwe.

Ndaki alisema wataka kupitia sheria zilizopo kuwapunguzia tozo ili kuwapunguzia mzigo wafanyabiashara hao.

Aldha, alimugiza Katibu Mkutu wa wizara hiyo na taasisi zake kuwa ondoa wetu wa katil maarufu 'zalajaja' katika minada kwa kuwa hawako kisheria.

Waziri huyo alisema watu hao wamekuwa wakiongeza gharama kubwa kwa wafanyabiashara wa mifugo, hivyo alivasihi wafanyabiashara wanunue mifugo kwa wafugaji na sio kwa galajaja.

Mfanyabiashara wa Mifugo, Elias Christopher, alidai tatizo finanza kwa usimamizi kwa viongozi kwa kutofuta sheria.

Christopher alisema nyama zinazuwa hivyo mitaani bila kufusta utaratibu na sheria zilizopo na kuwasababishia wakati mgumu wa kufanya biashara zao.

Mfanyabiashara mwingine, Shaban Magomba alisema, changamoto kubwa wanazokutana nazo ni Halmashauri kuwatoza ushuru zaidi ya mara mbili.

UVUVI



WAZIRI wa Mifugo na Uvuvu, Mashimba Ndaki, akizungumza na wafanyabiashara wa mifugo wa Mkoa wa Dar es Salaam, wakati akipokea kero za wafanyabiashara hao, mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo, Profesa Hezron Nonga. (Picha na Jumanne Guda).

Ubalozi Pakistan waipatia Hospitali ya Rufani Temeke gari la wagonjwa

Wafugaji waonywa kutumia dawa holela

Elizabeth Edward, Mwananchi
eedward@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Wawekeza-
ji katika sekta ya mifugo wam-
etakiwa kuzingatia vipimo vya
maabara kabla ya kumpa tiba ili
kuondoa uwezekano wa vimelea
vya ugonjwa kutengeneza usugu
wa dawa.

Ushauri huo umetolewa na
Meneja Mkuu wa wakala wa
Mabaara ya Mifugo Tanzania Dk
Omachi Geofrey, wakati akizin-

dua kituo cha huduma za mifugo
cha kampuni ya Interchick.

Alisema baadhi ya wafugaji
ji wana tabia ya kuipatia dawa
mifugo yao bila kufanya uchungu-
gizi kubaini kinachowasumbua
na dawa sahihi hali inayosababi-
sha mifugo kufa na madhara kwa
binadamu wanayokula nyama
husika.

Dk Geofrey alisema utafiti
walioufanya wamebaini kuwa
wadudu wengi wanaosumbua
mifugo wametengeneza usugu

dhidi ya dawa hivyo ni muhimu
kwa wafugaji kuwa makini na uto-
aji wa dawa kwa mifugo kwa kuz-
ingatia uchunguzi wa kimaabara.


Kwa upande wake daktari wa
mifugo wa kampuni ya Interchick
Birole Sanwa, alisema kituo walii-

**"Tafadhali wafugaji msitue
Watanzania wenzeni kwa
kutumia dawa bila kufuata
ushauri wa watalaaamu".**

Dk Omachi Geofrey

chokizindua kitamsaidia mfugaji
kufahamu chanzo cha ugonjwa
wa mnyama au wanyama wake ili
atambue dawa sahihi.

"Kama ilivyo kwa binadamu
sasa hivi tunaona hata kwa wan-
yama kuna tabia ya vimelea
kujenga usugu wa dawa, sasa
kupitia kituo hiki tunataka kupun-
guza tatizo hilo maana uchunguzi
wa magonjwa ya wanyama uta-
fanyika kwa kina kuwezesha kut-
ambua ni ugonjwa upi hasa kabla
ya kuutibu," alisema Dk Sanwa.



HONGERA

Kiiii chaaonoeata